**Jina:** ...................................................................... **Namba yako:** ..........................................

**Sahihi ya Mtahiniwa:** ................................................... **Tarehe:** ..................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**102/2**
**KISWAHILI**
**LUGHA**
**JULAI/AGOSTI 2013**
**MUDA: SAA 2 $^{1}/_{2}$**

# MTIHANI YA UTATHMINI WA PAMOJA WILAYA YA KIKUYU

## HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI KENYA (K.C.S.E)

**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**LUGHA**
**JULAI/AGOSTI 2013**
**MUDA: SAA $2^{1}/_{2}$**

**MAAGIZO**

Jibu maswali yote

Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

© 2013 KIKUYU DISTRICT INTERSCHOOLS
KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**1. UFAHAMU**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Maoni yetu juu ya uhuru tuliotwaa yanahitilafiana sana. Wao katika upande mmoja watu wanaofikiri kuwa kupewa uhuru ni kushikishwa upembo na kuambiwa: Haya jamaa oneni mitunda, pembeni mitunda mle mkasaze katika upande mwingine kuna wale wanaouona uhuru kama hali ya mtu kujihisi ana hiari na mamlaka ya juu ya jambo lolote lipasalo kutenda kwa mujibu wa maendeleo yake mwenyewe na ya jamaa kwa jumla. Kundi la tatu ni la wale wasiojua maana ya uhuru wao hukiri na kuitikia mara moja mawaidha wanayoshenezwa na viongozi wao.

Watu wa makundi haya matatu huwa hawana kosa kuwa katika hali waliyomo kwa kuwa hiyo ni hali ya kimaumbile. Uhuru una maana ya kujitawala na kujitawala kuna maana ya kujihami, kujikimu, kujivalisha na kujiamlia. Endapo baa hiyo ndiyo maana ya uhuru hapana budi kundi la kwanza kujibi swali hili, "matunda wanayokawia kupeana yamepandwa na nani?" Karima alimhuluku mwanadamu na kuupangia mastakimu yake kisha akamjalia akili, uwezo na vitu vya kumpa chakula. Maumbile nayo yakatwaa, wadhifa wa kuyabadili mazingira alimoishi mwanadamu. Hapo ughali wa maisha ukadhihirika. Kwa hivyo ikamlazimu kutumia akili na nguvu kupambana na vita vya kimaumbile ili kudumisha uhai.

Wanaochukua uhuru kuwa ni hali ya kujitegemea wana mawazo sadifu sana. Uhuru huweza kuelezwa katika sehemu mbili. Kwanza ni ile hali ya mtu kujikurupusha kutoka katika nyanyaso za mtu anayetawala kwa nguvu na kumtumikisha; ikiwa sasa hana ubwana juu yake. Pili ni kule kupewa hatamu na kuachwa pekee kumwendesha farasi usipomwendesha salama atakubwaga na kukuhasiri na mambo yatavurugika utakuwa umefuja. Tunao basi uhuru wa kimawazo na uhuru wa kiuchumi. Mawili haya hayaachani kama chungu na kia. Tukihisi kuwa tuko huru kimawazo tusiwe radhi na kuachia hapo. Hatuna budi pia kutazama upande wa uhuru wa kiuchumi.

Tulipoachiwa uamuzi wa mambo yetu wenyewe hakika tuliwekwa katika mizani kupimwa uwezo wetu wa kufanya kazi. Wajuzi wa mambo wamesema, "Uhuru ni kufanya kazi." Bila kufanya kazi kwa bidii uhuru hukosa maana. Uhuru una maana ya kujilimia mashamba, kustawisha ufugaji, kujijengea mashule, hospitali na vyumba vizuri vya kuishi, kujifundisha kuendelea kujitolea mhanga kazini na kuikuza jamii.

Kwa kuwa viongozi ni watu wanaotegemewa sana na wale wasiojua kujiendeleza, yabainika wanalo jukumu kubwa na gumu kuwaleta watu hao katika mkururo wa watu wengine. Walio na mawazo ya kufanyiwa kazi huku wao wataanasa, itawapasa kujiuliza mara moja, mara mbili kama wana uhuru wa kweli?

**Maswali**

a) Ipe taarifa hii kichwa mwafaka. (alama 1)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

b) Eleza kwa mukhtasari maana ya uhuru. (alama 4)

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

c) Kwa nini maana haieleweki kwa baadhi ya watu? (alama 4)

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

d) Sisi raia tulio huru tuna wajibu gani katika taarifa? (alama 1)

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

e) Fafanua wajibu wa viongozi katika taifa huru. (alama 2)

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

f) Eleza maana ya msamiati na vifungu vifuatavyo kama yalivyotumiwa katika taarifa. (alama 3)

(i) Kushikishwa upembo ukapambe matunda.

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

(ii) Kula na kusaza

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

(iii) Huku wao wataanasa

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

## 2. MUKHTASARI

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha husitawisha ufahamu wetu wa mambo tusomayo. Mazoezi katika kuandika husitawisha ufahamu katika kusoma kwa sababu katika kuandika ni lazima tujaribu kuyatumia maneno vizuri na kufahamu ugumu wa usemi. Twajifunza matumizi ya lugha katika kuzungumza na kuwasikiliza wengine wakizungumza. Lugha tusomayo ikiwa imeandikwa hasa huwa ni aina ya lugha ya mazungumzo vile vile. Kuna ujuzi mwingi katika kuzungumza upatikanao katika shule - kama vile michezo ya kuigiza, hotuba, majadiliano na mazungumzo katika darasa na haya yote husaidia katika uhodari wa matumizi ya lugha.

Ujuzi wa kila siku hutasaidia katika maendeleo ya kusoma na usitawi wa msamiati. Ikiwa mwanafunzi amemwona ndovu hasa, atakuwa amejua maana ya neno ndovu vizuri zaidi kuliko mwanafunzi ambaye hajapata kumwona ndovu bali ameelezwa tu vile alivyo. Vile vile ujuzi wa kujionea sinema au michoro husaidia sana katika masomo. Kwa hivyo kwa njia fulani mambo yote juu ya ujuzi wa kila siku husaidia kufahamu mambo yaliyoandikwa. Ikiwa mwanfumzi ana huzuni au ana furaha, akiwa mgonjwa au amechoka au amesifiwa, haya yote ni ujuzi. Wakati ujao mwanafunzi asomapo juu ya mtu ambaye amepatikana na mambo kama hayo hana budi kufahamu vizuri zaidi.

Karibu elimu yote ulimwenguni huwa imeandikwa vitabu lakini lugha zote hazina usitawi sawa kuhusu fasihi. Kwa bahati mbaya lugha nyingine hazijastawi sana na hazina vitabu vingi lakini katika lugha nyingine karibu mambo yote yanayohusiana na elimu huweza kupatikana katika vitabu. Inambidi mwanafunzi anayejifunza asome vitabu au majarida juu ya sayansi au siasa au historia, lakini haimbidi kusoma tu juu ya taaluma fulani anayojifunza. Inafaa asome juu ya michezo, mambo ya shani, na juu ya mahali pageni ili kupata ujuzi wa mambo mengi mbali mbali.

**Maswali:**

a) Fupisha aya za kwanza mbili kwa kutumia maneno 65. (alama 8, 1 ya utiririko)

Matayarisho:

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

Jibu:

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

b) Kwa kuzingatia habari zote muhimu na bila kupoteza maana asilia, fupisha aya ya mwisho. (maneno 30)

(alama 5, 1 ya utiririko)

Matayarisho:

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

Jibu:

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

## 3. MATUMIZI YA LUGHA.

a) Ni ala zipi za sauti zinazotumika kutamkia sauti zifuatazo? (alama 3)

/I/

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

/ng'/

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

/ny/

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

b) Ainisha sentensi ifuatayo: (alama 3)

Aliyefiwa

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

c) Eleza matumizi ya "ni" katika sentensi zifuatazo: (alama 3)

(i) Wanasoka wanauchezea mpira uwanjani.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(ii) Kiptoo ni mkulima hodari

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(iii) Halima alinitembelea kwetu juzi

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

d) Tunga sentensi inayodhihirisha matumizi ya ngeli ya U - U. (alama 1)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

e) Andika kwa wingi: (alama 2)

Kifaru huyu na kondoo yule ni wa mfugaji yupi?

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

g) Tumia maneno kwenye njozi ifuatayo kuonyesha maana tofauti katika sentensi. (alama 2)

(i) Suka

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(ii) Zuka

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

h) Tofautisha matumizi ya "vizuri" katika sentensi hii. (alama 2)

Alinunua viatu vizuri na akafungiwa vizuri.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

i) Bainisha shamirisho kipozi na shamirisho ala kutokana na sentensi ifuatayo. (alama 2)

Mtoto alikunywa uji kwa kijiko.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

j) Andika sentensi hii katika msemo halisi. (alama 2)

Mwalimu alimwambia mwanafunzi malize kazi hiyo haraka.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

k) Tambua hali zilizotumika katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Mwizi huvunja nyumba wakati watu wamelala.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

l) Andika maneno yafuatayo katika kauli zilizoonyeshwa katika mabano. (alama 2)

| **Neno** | **Kauli** | **Jibu** |
|---|---|---|
| Kunja | (kutenduka) | .................................................. |
| Safari | (kutendesheka) | .................................................. |

m) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii. (alama 2)

Anapenda kusoma kuliko Rehema.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

n) Yakinisha sentensi ifuatayo. (alama 1)

Nchi za Afrika Mashariki hazikulemewa na madeni.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

o) Geuza sentensi uliyopewa iwe katika hali ya udogo. (alama 2)

Nyumba yenyewe ilijengwa karibu na mto unaofurika mara kwa mara.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

p) Bainisha aina ya chagizo katika sentensi hii. (alama 2)

Alimkimbilia adui kishujaa kabla ya kumwangamiza.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

q) Kamilisha jedwali (alama 2)

| **Kitenzi** | **Kivumishi** |
|---|---|
| Samehe | ................................................................ |
| ........................................................ | karimu |
| Kakamaa | ................................................................ |
| ........................................................ | utulivu |

r) Akifisha sentensi ifuatayo. (alama 3)

Mwalimu alipoingia ukumbini alituambia kimya au niwaadhibu

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

**4. ISIMU JAMII**

a) Eleza sababu nne zinazowafanya watu kubadili msimbo. (alama 4)

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

b) Mazungumzo ya mahakamani husheheni sifa zipi. (alama 6)

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................